

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA
SHULE YA SEKONDARI YA KILIMO KILOSA
S.L.P. 145 KILOSA MOROGORO
Barua pepe: mkuukilosa2020@gmail.com

NAMBA ZA SIMU
Mkuu wa shule 0621353768 / 0717015950
Makamu Mkuu wa Shule 0715249810 / 0629914753

KUMB. NA: SSK/J/I/2021
MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI.....
S.L.P.....
.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA
SEKONDARI YA KILIMO YA KILOSA WILAYA YA KILOSA MKOA MOROGORO
MWAKA 2021**

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** mwaka **2021** katika shule yetu. Shule ya sekondari ya kilimo kilosa ipo umbali wa km 26 kutoka halmashauri ya wilaya Kilosa katika mkoa wa Morogoro. Kuna njia mbili za usafiri zitakazo kufikisha shule ya Sekondari ya Kilimo Kilosa.

Mosi, **usafiri wa gari moshi(treni ya reli ya kati)**. Tunashauri watakao amua kutumia njia hii kutoka Kigoma na Mwanza washuke stesheni ya kilosa. Nenda stendi ya mabasi ya wilaya ya kilosa, Panda gari zinazokwenda Dumila. Shuka kituo cha Rudewa(nauli ni tsh 3000 tu). Chukua bodaboda wakulete kilosa sekondari(kizunguzi) na nauli ya bodaboda ni Tsh 2000 tu.

Pili, **usafiri wa mabasi** kwa watakaotumia njia inayopitia mkoa wa DODOMA washuke kituo cha Dumila. Ulizia stendi ya magari yanayo kwenda kilosa, Panda gari hiyo inayoenda kilosa halafu shuka

kituo•cha Rudewa(nauli ni Tsh 4000/=). Chukua bodaboda hadi shulen. Kwa watakao tumia njia inayo pitia Chalinze(Pwani) na mkoa wa Iringa, shuka kituo cha mabasi cha mkoa wa Morogoro(MSAMVU).

Panda gari ya kilosa kupitia Dumila na shuka kituo cha Rudewa(Nauli ni Tsh 6000) panda bodaboda hadi shule.

Muhula wa kwanza kwa mwaka wa msomo 2021 unaanza tarehe 11/01/2021 mwanao anatakiwa Kuripoti shulen. tarehe 09/01/2021 au tarehe 10/01/2021 ili tarehe 11/01/2021 awe darasani akihudhuria masomo.

Aidha Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu Sanyansi na Teknolojia,yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za shule

(a) (i) Aje na Suruali mbili za rangi ya damu ya mzee iwe na marinda mawili kulia na mawili kushoto isiwe ya kubana yaani “Model” upana chini usipungue sentimeta 16. kwa watakaoshindwa kushona nyumbani waje na fedha shulen. wataelekezwa na idara ya malezi kwa mafundi wa jirani ambapo gharama ya suruali moja ni shilling elfu ishirini(20,000/=) tu.

(ii)Aje na Suruali mbili za kuvaan nje ya darasa rangi ya (Dark Blue) iwe na marinda mawili kulia na mawili kushoto isiwe ya kubana yaani “Model” upana chini usipungue sentimeta 16. kwa watakaoshindwa kushona nyumbani waje na fedha shulen. wataelekezwa na idara ya malezi kwa mafundi wa jirani ambapo gharama ya suruali moja ni shilling elfu ishirini(20,000/=) tu.

iii) Mashati mawili au zaidi meupe ya mikono mifupi yasiyo bana au pwaya sana mwili.

iv) Viatu vyeusi vya kufunika vya kamba. Viatu vya mtindo wa magorofa au mabuti haviruhusiwi

v) Soksi nyeusi pea mbili au Zaidi.

vi) Mabuti ya mvua (gum boots).

vii) T-shirts 2 za njano (zisizo na maandishi aina ya timberland zenyenye shido ya duara) za kushindia.

viii) Sweta la bluu lenye shingo ya V.

ix) Tai (hii inapatikana maeneo ya shule gharama yake ni shilling 5,000/=)

(b) Sare ya michezo kwa shule hii ni kama ifuatavyo;

i)Bukta ya rangi ya blue au nyekundu na jezi yake inayo fanana rangi na bukta isiwe na maandishi yoyote.

ii)Viatu vya raba (canvas shoes) na viatu vya kuchezea mpira wa miguu.

iii) Track suit ya blue au nyekundu

2.2 Mahitaji ambayo mwanafunzi inabidi aje nayo kwa matumizi yake.

- a) Tranka (sanduku la bati lenye kufuli imara kwa ajili ya kuhifadhi vitu vyake.
- b) Godoro la upana wa futi $2\frac{1}{2}$. Maeneo karibu na shule yanauzwa 45000/=
- c) Mathematical set, rula, kalamu, daftari kubwa zisizopungua 15 (counter books
- d) Sahani, kikombe, bakuli na kijiko.
- e) Ndoo moja (lita 10) na galoni ya lita 5 ya kutunzia maji ya kunywa.
- f) Shuka mbili (**light blue/blue isiyokolea**).
- g) Blanketi moja.
- h) Chandarua (ni lazima). Hii ni sehemu yenyе mbu wengi.
- i) Fulana ya ndani(singlet) nyeupe mbili au Zaidi.
- j) Leso (handkerchief) na Taulo.
- k) Nguo za ndani(boxer) zisipungue tatu.

**N.B Nguo za nyumbani haziruhusiwi hivyo ni vyema mwanafunzi aje akiwa amevaa sare za shule.
Mitindo ya kunyoa kiduku haikubariki shulenii kwetu.**

3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995, inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu Sanyansi na Teknolojia,yenyе dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Rais TAMISEMI yenyе jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu.

3.1 KANUNI ZA LAZIMA KUFUATWA NA WANAFUNZI WOTE SHULENI

- a) Kula chakula cha shule.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ya ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya mazingira ndani ya shule
- f) Kutunza usafi wa mwili,mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote uwapo shule na wakati wa kusafiri kutoka na kurudi shulenii.
- h) kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- i) Kutunza mali za umma kwa uaminifu na kwa uzalendo .
- j) Heshima kwa viongozi ,wazazi ,wafanyakazi wote ,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

3.2) MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.

a) Hairusiwi kumiliki simu au line ya simu ya aina yoyote shulenii.

- b) Wizi
- c) Uasherati na ushoga
- d) Ubakaji
- e) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaa kama vile uvutaji bangi,cocaine; mirungi,kubeli na kadhalika
- f) Kupigana au kupiga
- g) kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- h) Kudharau bendera ya Taifa

- i) kuoa au kuolewa
- j) Kugoma,kuchochaea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu;
- k) Kukataa adhabu kwa makusudi
- l) Kufanya au jaribio la kuua au kujiua au kutishia kujiua au kuua mwezako.
- m) Kushiriki matendo ya kiharifu yanayo pelekea kuvunja sheria za nchi.
- n) Kutoa lugha chafu kwa jamii kwa ujumla wake.
- o) Utoro wa darasani na katika kazi za nje ya madarasa.
- p) Kuvuka mto Wami unaozunguka eneo la shule. Mto huu ni hatari una mamba na viboko.
- q) Kutovaa nguo za shule mwanafunzi akiwa safarini kuja shuleni au akiwa shuleni.

4.0 Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

- (a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.(**KIAMBATANISHO NAMBA 2**)
- (b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na tamko rasmi la kukubaliana sheria na taratibu za shule.. (**KIAMBATANISHO NAMBA 01**)
- (c) Fomu ya mwanafunzi kukiri kukubaliana na sheria,kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule. (**KIAMBATANISHO NAMBA 03**)

5.0

HITIMISHO

Shule yetu ni shule ya kilimo hivyo mwanaao anatakiwa awe tayari kushiriki na kupenda masuala yanayo husiana na kilimo.Hakikisha mzazi au mlezi umesoma kwa umakini fomu hii na kujadiliana na mwanaao utayari wake katika kuzingatia yaliyo tajwa kwenye fomu hii.

Utunzaji wa mazingira na kushiriki shughuri zingine zenyenye kuhamasisha Uzalendo kwa nchi yetu ni lazima ikiwemo kushiriki katika vikundi mbalimbali hapa shuleni mfano; MALI HAI CLUB, PCCB, FEMA, SCOUT n.k

Karibu sana,




**MBARAKA M. KUPELA.
MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI YA KILIMO KILOSA
S.L.P. 145
KILOSA

SHULE YA SEKONDARI YA KILOSA

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA KUKUBALI SHERIA NA
NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA**



Bandika picha
hapa
(yenye shati jeupe)

1. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

A. Jina kamili la mwanafunzi

- a) Jina la kwanza
- b) Jina la baba
- c) Jina la ukoo.....

B. Tarehe ya kuzaliwa..... mwezi mwaka

(ambatanisha nakala ya cheti cha kuzaliwa)

C. Mahali alipozaliwa Mkoa Wilaya

KataKijiji/Mtaaa.....

D. Mwanafunzi huyu SIYO YATIMA / YATIMA (Kama ni YATIMA BABA
AMEFARIKI AU MAMA AMEFARIKI AU WAZAZI WOTE
WAMEFARIKI.)

E. Uraia: MTANZANIA / SIYO MTANZANIA
(Ambatanisha cheti cha kuzaliwa)

F. MAWASILIANO YA MZAZI AU MLEZI WA MWANAFUNZI

Namba ya simu 1..... MLEZI/MZAZI
Namba ya simu 2..... MLEZI/MZAZI
Namba ya simu 3.....(JIRANI YAKO)
Namba ya simu 4.....(AFISA
MTENDAJI MTAAC/KIJINI)

SAINI NA MUHURI WA MTENDAJI WA MTAAC/KIJINI.

- G. Jina la shule ya Msingi Uliyosoma
 Namba ya mtihani taifa ya darasa la saba
 Prem Namba ya mwanafunzi

(Taarifa hizi zinapatikana kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi alipo soma mwanafunzi, Zijazwe kwa usahihii)

2. TAARIFA YA MZAZI/MLEZI

- A. Jina la Mzazi/Mlezi.....
 B. Namba ya kitambulisho cha Taifa
 C. Kazi ya Mzazi/Mlezi.....
 D. Anwaani ya Mzazi/Mlezi: S.L.PENEO.....
 E. Mawasiliano:.....,

(Andika namba zote ulizonazo zinazopatikana muda wote)

- F. Mtoto wangu ni MLEMAVU/SIYO MLEMAVU (Kama ni mlemavu taja aina ya ulemavu wake)

- G. Ndugu ninaowaruhusu kumtembelea mwanafunzi huyu awapo shulenii ;
 a)uhusiano
 b)uhusiano
 c)uhusiano
 d)uhusiano
 e)uhusiano

(Ndugu wengine wote hadi nitoe idhini ya maandishi mimi Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi huyu)

- H. Elimu ya Mzazi/ Mlezi:.....

KIAMBATANISHO NAMBA 02

KILOSA AGRICULTURAL SECONDARY SCHOOL

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

FORM: The Medical Officer,

Government Hospital.....

.....
.....
.....

TO: The Headmaster,
Kilosa Agricultural Secondary School,
P. O. Box 145,
KILOSA.

RE: MEDICAL CERTIFICATE

(TO BE COMPLETED BY A GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)

I have examined.....(mention three names) who wish to join
Form I in your school as follows:-

AREA	REMARKS
1. Skin
2. Eyes
3. Ears
4. Teeth
5. Chest
6. Spleen
7. Abdomen
8. Urine
9. Stool
10. HB Haemoglobin
11. Inoculation against meningitis
12. Sickle cell
13. Asthma
14. Any other comments
15. Blood Group

I consider that he is physically/not physically fit to join your school.

Signature.....

Date.....

Official stamp.....

(KIAMBATISHO NA 3.)

TAMKO RASMI LA KUSOMA NA KUELEWA TARATIBU ZOTE ZA SHULE YA SEKONDARI YA KILIMO KILOSA

1. MWANAFUNZI

Mimi(Taja majina yote matatu), Nimesoma kwa makini na kuyaelewa maelekezo yote ya SHULE YA SEKONDARI YA KILIMO KILOSA kwa hiyo nakubali kuipokea/sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. Ninaahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule na kujifunza kwa bidii.

Kwa kuwa nimekubaliana na taratibu zote za shule, natamka wazi bila kushurutishwa na mtu kwamba nitazifuta taratibu zote na sitakuwa sehemu ya vurugu yoyote au mgomo wowote hapa shulenii.

Tarehe..... Sahihi.....

2. MZAZI/MLEZI:

Nimehakikisha mwanangu amezisoma na kuzielewa sheria za shule nanimemesisitiza katika hilo. Nakiri kwamba tumenita kipengele kwa kipengele

Tarehe

Jina

Saini.....

**3. MAELEZO MENGINE MUHIMU YANAYO MUHUSU MWANAFUNZI AMBAYO SHULE
INAPASWA KUFAHAMU ILI KUWEZA KUMSAIDIA MWANAFUNZI HUYU.**